TBARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE (SFNA) 2015

## 06 STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE MWAKA 2015

# 06 STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO

*Kimechapishwa na*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624,
Dar es Salaam, Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2016

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI ........................................................................................................ iv
1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1
2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI .................................... 2
2.1 Sehemu A: Stadi za Kazi ........................................................... 2
2.2 Sehemu B: Haiba na Michezo ................................................... 25
3.0 TATHMINI YA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA MADA …41
4.0 HITIMISHO .......................................................................................... 41
5.0 MAPENDEKEZO .................................................................................. 42
Kiambatisho A ............................................................................................ 44
Kiambatisho B ............................................................................................ 46

## DIBAJI

Taarifa ya uchambuzi wa majibu ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne 2015 kwa masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo imeandaliwa kwa lengo la kutoa mrejesho kwa wanafunzi, walimu, watungasera, watunga mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna wanafunzi walivyojibu maswali ya upimaji huo. Majibu ya wanafunzi katika upimaji ni kiashiria kimojawapo kinachoonesha mambo ambayo wanafunzi walijifunza kwa ufasaha na yale ambayo hawakujifunza kwa ufasaha katika kipindi cha miaka minne ya Elimu ya Msingi.

Katika kitabu hiki, mambo mbalimbali ambayo yamechangia wanafunzi kushindwa kujibu maswali kwa usahihi yameainishwa. Uchambuzi unaonesha kuwa yafuatayo yamechangia kuwafanya wanafunzi washindwa kujibu maswali kwa usahihi: kushindwa kuelewa maelekezo ya swali, kuwa na uelewa mdogo wa mada mbalimbali katika somo na njia za ufundishaji, na ujifunzaji unaoegemea zaidi nadharia kuliko vitendo. Uchambuzi kwa kila swali umefanyika ambapo dosari mbalimbali zilizojitokeza wakati wanafunzi walipokuwa wanajibu maswali yao zimeainishwa kwa kuonesha idadi ya wanafunzi waliojibu maswali kwa usahihi, walioshindwa kuandika jibu sahihi, na ambao hawakujibu maswali. Sababu zilizochangia kuchagua majibu yasiyo sahihi zimetolewa kwa kila swali.

Baraza la Mitihani la Tanzania lina imani kuwa mrejesho uliotolewa utawawezesha wadau mbalimbali wa elimu kuchukua hatua muhimu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa lengo la kupatia ufumbuzi dosari zilizoainishwa katika taarifa hii. Aidha, Baraza la Mitihani lina imani kuwa endapo maoni yaliyotolewa yatafanyiwa kazi ipasavyo, ujuzi na maarifa

watakayopata wanafunzi wanaopimwa darasa la nne yataongezeka na hatimaye kiwango cha ufaulu katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kitaongezeka pia.

Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kutoa shukrani za dhati kwa Maafisa Mitihani, Watahini, Wafanyakazi wa Idara ya TEHAMA, na wote waliohusika, kwa mchango na juhudi zao zilizofanikisha uandaaji wa taarifa hii.

Mwisho, Baraza litashukuru kupokea maoni na mapendekezo kutoka kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu kwa ujumla ambayo yatalenga kuboresha taarifa za uchambuzi wa maswali ya Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa siku zijazo.



Dkt. Charles E. Msonde

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo ulifanyika Novemba 2015. Idadi ya wanafunzi waliofanya upimaji ilikuwa 950,304 ambao ni sawa na asilimia 94.1 ya wanafunzi wote waliosajiliwa. Uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika maswali ya upimaji huu unaonesha kwamba wanafunzi 801,229 (84.3%) walifaulu.

Karatasi ya maswali ya upimaji wa mwaka 2015 kwa masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo ilikuwa na maswali 25 ambayo yalikuwa yamegawanywa katika sehemu mbili: A na B. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote na kila swali lilikuwa na alama mbili. Sehemu A ilihusu Stadi za Kazi na ilikuwa na maswali saba ya kuchagua jibu sahihi; maswali matano ya kuoanisha; na maswali matatu ya majibu mafupi. Sehemu B ambayo ilihusu Haiba na Michezo ilikuwa na maswali saba ya kuchagua jibu lililo sahihi na maswali matatu ya majibu mafupi. Katika maswali ya kuchagua, wanafunzi walitakiwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika chaguzi nne walizopewa na kuandika herufi ya jibu sahihi katika kisanduku walichopewa. Katika maswali ya kuoanisha wanafunzi walitakiwa kuoanisha maswali ya Fungu A na majibu katika Fungu B na kisha kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano waliyopewa. Maswali ya majibu mafupi yaliwataka wanafunzi kujaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuandika neno sahihi ili kuifanya sentensi husika kuwa kamili na sahihi.

Taarifa hii inachambua majibu ya wanafunzi katika kila swali. Uchambuzi utabainisha maelekezo ya kila swali, ufaulu wa wanafunzi, na sababu za ufaulu huo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI

### 2.1 Sehemu A: Stadi za Kazi

**Swali la 1 - 7: Maswali ya Kuchagua Jibu Sahihi**

**Swali la 1:** Aina mbili za unamu ni

A mwembamba na mnene


B mzito na mwepesi

C mdogo na mkubwa

D kwaruzi na mwororo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi wa kubaini aina za unamu. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walihitaji kuwa na uelewa wa kutosha wa kutambua aina mbalimbali za unamu.

Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu jumla ya wanafunzi 227,227 (asilimia 23.91) walichagua jibu sahihi D "Kwaruzi na mwororo", wakati wanafunzi 722,810 (asilimia 76.06) walichagua kati ya vipotoshi A "mwembamba na mnene", B "mzito na mwepesi" na C "mdogo na mkubwa". Hata hivyo, wanafunzi 265 (asilimia 0.03) hawakujibu swali hili. Chati Na. 1 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 1**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 1 ulikuwa hafifu.

Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu maana ya neno unamu na mionekano ya nyuso za vitu halisi, michoro au picha. Baadhi ya wanafunzi katika kundi hili walichanganya sifa za jumla na mionekano ya nyuso za vitu. Kwa mfano, wanafunzi hawa walishindwa kujua kuwa mwonekano wa nyuso na mbao inaweza kuwa kwaruzi au nyororo lakini sio ndogo au kubwa. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na maarifa kuhusu unamu.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walielewa kuwa mwonekano wa nyuso za vitu halisi, picha au michoro unaweza kuwa kwaruzi au mwororo. Hii ilidhihirisha kuwa waliweza kutambua kuwa mwonekano wa vyuso za vitu halisi kama ubao huweza kuhisiwa kuwa kwaruzi au mwororo.

**Swali la 2:** Usafi na usalama ni kanuni kuu katika

A upakuaji wa vyakula

B upishi wa vyakula

C ulaji wa vyakula

D uzalishaji wa vyakula.

Swali lilitoka katika mada ya *Upishi*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu kanuni za usafi na usalama katika upishi. Ili kuweza kujibu swali hili kwa usahihi, wanafunzi walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kanuni kuu za usafi na usalama zinazotakiwa kufuatwa katika shughuli zote za kuandaa vyakula.

Jumla ya wanafunzi 519,437 (asilimia 54.7) walichagua jibu sahihi B "upishi wa vyakula" wakati wanafunzi 430,718 (asilimia 45.3) walichagua kati ya vipotoshi A "upakuaji wa vyakula", C "ulaji wa vyakula" na D "uzalishaji wa vyakula". Aidha, wanafunzi 145 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 2.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 430,718 | 519,437 | 145 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 45.3 | 54.7 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walibaini kuwa usafi na usalama ni kanuni kuu wakati wa kuandaa na kupika chakula. Walielewa pia kuwa ni muhimu kuzingatia kanuni za usafi na usalama ili kuzuia ajali, hasara na madhara yanayotokana na kutofuata kanuni hizo.

Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi walishindwa kubaini shughuli ambayo kanuni za usafi na usalama zinatakiwa kufuatwa. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu kanuni za upishi wa vyakula.

**Swali la 3:** Mara baada ya kuchukua vipimo, mshonaji wa nguo anatakiwa

A kuchora vipimo katika vigezo

B kuandaa meza ya ushoni

C kushona vigezo

D kukata vigezo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ushoni wa nguo*. Swali lililenga kupima ufahamu wa wanafunzi kuhusu ushonaji wa nguo. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua zinazopaswa kufuatwa wakati wa kushona nguo.

Jibu sahihi A "kuchora vipimo katika vigezo" lilichaguliwa na wanafunzi 477,997 (asilimia 50.3) wakati wanafunzi 472,191 (asilimia 49.7) walichagua kati ya vipotoshi B "kuandaa meza ya ushoni", C "kushona vigezo" na D "kukata vigezo". Hata hivyo, wanafunzi 109 hawakujibu swali hili. Jedwali Na. 2 linaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 2**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 3.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 472,191 | 477,997 | 109 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 49.7 | 50.3 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi A “kuchora vipimo katika vigezo” walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu hatua za ushonaji wa nguo. Walifahamu kuwa baada ya kuchukua vipimo, fundi wa nguo hupaswa kuchora vigezo kwa kutumia vipimo alivyochukua kabla ya kukata na kushona nguo.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua vipotoshi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu hatua za ushonaji wa nguo. Kwa mfano, wanafunzi waliochagua kipotoshi B “kuandaa meza ya ushoni” hawakuelewa kuwa meza ya ushoni huandaliwa mapema kabla mshonaji hajachukua vipimo. Meza hii hutumika wakati wa kuchora kigezo pamoja na kukata kitambaa. Wanafunzi waliochagua kipotoshi C “kushona vigezo” hawakuwa na uelewa kuwa kigezo hakiwezi kushonwa kwa sababu ni kielelezo cha jinsi ya kukata nguo. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D “kukata vigezo” hawakuelewa kuwa baada ya kuchukua vipimo, hatua inayofuata ni kuchora vigezo na si kukata kigezo. Wanafunzi hawa hawakuelewa kuwa ni baada ya kuchora vigezo ndipo mshonaji hukata na kushona nguo. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu hatua za ushonaji wa nguo.


**Swali la 4:** ________________huboresha sauti wakati wa kuimba.

A Beti
B Redio
C Gitaa
D Kinasa sauti.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Muziki*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu aina za ala za muziki zinazotumika

kuboresha sauti wakati wa kuimba. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kazi za ala mbalimbali za muziki zinazotumika wakati wa kuimba.

Jumla ya wanafunzi 312,860 (asilimia 32.92) walichagua jibu sahihi C “gitaa” wakati wanafunzi 637,324 (asilimia 67.07) walichagua kati ya vipotoshi A “beti”, B “redio” na D “kinasa sauti”. Wanafunzi 115 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama Chati Na. 2 inavyoonesha.




**Chati Na. 2**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 4 ulikuwa wa wastani.

Baadhi ya wanafunzi waliochagua kipotoshi A “beti” walishindwa kuelewa matakwa ya swali. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B “redio” walijua kuwa redio hutoa sauti ila walishindwa kuelewa kuwa sauti ya redio haiwezi kuboresha sauti wakati wa kuimba. Waliochagua kipotoshi D “kinasa sauti” hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vifaa vya muziki na kazi zake hivyo walioanisha maneno “kunasa sauti” na neno “sauti” lililokuwa kwenye shina la

swali. Aidha, wanafunzi hawa walidhani sauti huboreshwa wakati wa kurekodi. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu matumizi ya ala za muziki.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu kazi za ala mbalimbali za muziki. Walielewa kuwa gitaa linapopigwa kitaalamu huboresha sauti za waimbaji pamoja na zile zinazotolewa na ala nyingine.

**Swali la 5:** Tunatumbukiza kindu kwenye maji ili

A kuzisafisha
B kuzilainisha
C kuzifanya ziwe ndefu
D kuongeza rangi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Ususi*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu sababu za kutumbukiza kindu kwenye maji kabla ya kusuka kili. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua za kuandaa kindu kabla ya kuzisuka.

Jumla ya wanafunzi 454,200 (asilimia 47.8) walichagua jibu sahihi B “kulainisha” wakati wanafunzi 495,991 (asilimia 52.2) walichagua kati ya vipotoshi A “kusafisha”, C “kuzifanya ziwe ndefu” na D “kuongeza rangi”. Hata hivyo, wanafunzi 110 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 3.

**Jedwali Na. 3**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali na 5.

| Alama | Waliokosa | Waliopata | Wasiojibu |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 495,991 | 454,200 | 110 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 52.2 | 47.8 | 0 |

Wanafunzi waliochagua kipotoshi A “kusafisha” walioanisha “maji” na “kusafisha” na hawakukumbuka kuwa kindu hazisafishwi kwa maji kabla ya kufumwa. Aidha, wanafunzi waliochagua kipotoshi C “kuzifanya ziwe ndefu”, walishindwa kuelewa kuwa kindu ni sehemu ya mmea iliyokatwa hivyo haiwezi kuongezwa urefu. Wanafunzi waliochagua D “kuongeza rangi” walishindwa kuelewa kuwa maji ambayo hayakutiwa rangi hayawezi kuongeza rangi katika kindu. Wanafunzi wengine walichanganya kati ya ulainishaji na utiaji rangi kindu kwa sababu njia zote mbili zinahusisha kuchovya kindu katika maji yasiyo na rangi kwa ajili ya kulainisha na yenye rangi kwa ajili ya kutia rangi. Wanafunzi hawa na wale ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu hatua zinazotakiwa kufuatwa katika kuandaa kindu kabla ya kuzisuka na matumizi ya maji katika maandalizi hayo.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa bayana kuhusu hatua za kutayarisha kindu kabla ya kuzisuka. Wanafunzi hao walielewa kuwa maji hufanya kindu kuwa laini na hivyo kuzifanya zisikatike wakati wa kusuka kili.

**Swali la 6:** Kengele, pembe, tarumbeta na filimbi ni ala zinazotumika kucheza

A majigambo

B shairi

C ngoma za asili

D ngonjera.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Sanaa za Maonyesho*. Swali lilipima uelewa wa wanafunzi kuhusu aina za ala zinazotumika katika aina mbalimbali za sanaa za maonyesho. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu ala na matumizi yake katika aina mbalimbali za sanaa za maonyesho.

Jumla ya wanafunzi 608,974 (asilimia 64.1) walichagua jibu sahihi C "ngoma za asili" wakati wanafunzi 341,236 (asilimia 35.9) walichagua kati ya vipotoshi A "majigambo", B "shairi" na D "ngonjera". Hata hivyo, wanafunzi 88 hawakujibu swali hili. Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 4.

**Jedwali Na. 4**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 6.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 341,236 | 608,974 | 88 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 35.9 | 64.1 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za ala za muziki na sehemu zinakoweza kutumika. Kwa hiyo, katika kundi hili waliweza kubainisha sanaa za

maonyesho ambazo hazitumii ala za muziki kama vile majigambo, mashairi, pamoja na ngonjera.

Wanafunzi waliochagua majibu yasiyo sahihi hawakuwa na uelewa wa kutosha ama kuhusu aina za ala za muziki au aina za sanaa za maonyesho. Walishindwa kuelewa kuwa kila aina ya sanaa inatumia ala tofauti ilhali sanaa zingine kama vile majigambo, mashairi na ngonjera hazitumii ala. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu ala zinazotoa sauti.

**Swali la 7:** Tunafua nguo ili

A kuondoa uchafu


B kuongeza harufu nzuri

C kuondoa rangi

D kuongeza mng'aro.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Udobi*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhumuni la kufua nguo. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu hatua mbalimbali za utunzaji wa nguo na faida za kila hatua.

Jumla ya wanafunzi 810,176 (asilimia 85.25) walichagua jibu sahihi A "kuondoa uchafu", wakati wanafunzi 140,051 (asilimia 14.74) walichagua kati ya vipotoshi B "kuongeza harufu nzuri", C "kuondoa rangi" na D "kuongeza mng'aro". Hata hivyo, wanafunzi 70 (asilimia 0.01) hawakujibu swali hili. Chati Na. 3 inaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri.




**Chati Na. 3**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 7 ulikuwa mzuri.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walielewa dhumuni la kufua nguo. Hii inaonesha kuwa wanafunzi hao walielewa vizuri mada ya udobi. Hali hii inaweza kuwa ilitokana na wanafunzi hao kuwa na uzoefu kutoka nyumbani kwao, ama kwa wao wenyewe kufua au kuwaona wengine wakifua nguo.

Wanafunzi waliochagua kipotoshi B “kuongeza harufu nzuri” walihusisha tendo la kufua na harufu nzuri inayotokana na baadhi ya sabuni za kufulia zenye manukato. Wanafunzi waliochagua kipotoshi C “kuondoa rangi” huenda huona baadhi ya nguo zinapofuliwa hutoa rangi. Hivyo, walifikiri kuwa sababu ya kufua nguo ni kuondoa rangi. Wale waliochagua kipotoshi D “kuongeza mng’aro” walishindwa kutofautisha mwonekano wa nguo wa “kutakata” na “kung’ara” kwa nguo iliyofuliwa. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walishindwa kubainisha sababu ya kufua nguo.

**Swali la 8 – 12: Maswali ya Kuoanisha**

**Maswali Na. 8 – 12** yalitoka katika mada ya *Kilimo*, *Ufugaji na Uvuvi*. Maswali haya yalilenga kupima uwezo wa wanafunzi wa

kutumia maarifa yao kuainisha aina mbalimbali za mboga. Ili wanafunzi waweze kujibu maswali haya kwa usahihi, walitakiwa kuwa na maarifa kuhusu makundi mbalimbali ya mboga na mifano ya mboga katika kila kundi.

**Maswali na majibu ya swali la 8 – 12.**

| | **Fungu A** | **Herufi** | **Fungu B** |
|---|---|---|---|
| 8. | Mboga za aina ya matunda | (    ) | A Spinachi |
| 9. | Mboga za aina ya mizizi | (    ) | B Vitunguu saumu |
| 10. | Mboga za aina ya majani | (    ) | C Viazi mviringo |
| 11. | Mboga za aina ya maua | (    ) | D Njegere |
| 12. | Mboga za aina ya mbegu | (    ) | E Nyanya |
| | | | F Koliflawa |
| | | | G Karoti |

**Swali la 8:** Mboga za aina ya matunda (    )

Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini mboga za aina ya matunda.

Jumla ya wanafunzi 390,579 (asilimia 41.1) walichagua jibu sahihi E "Nyanya" wakati wanafunzi 559,503 (58.9%) walichagua kati ya vipotoshi A "spinachi", D "njegere", na G "karoti". Idadi ya wanafunzi ambao hawakujibu swali hili ni 219. Jedwali Na. 5 linaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 5**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 8.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 559,503 | 390,579 | 219 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 58.9 | 41.1 | 0 |

Wanafunzi waliochagua A "spinachi" walishindwa kuelewa kuwa spinachi ni mboga za majani na siyo matunda. Wanafunzi waliochagua kipotoshi D "njegere" walishindwa kutofautisha matunda na mbegu. Wale waliochagua G "karoti" walichanganya karoti na matunda kutokana na kuwa na rangi kama ya matunda yaliyoiva. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walidhihirisha kutokuwa na ujuzi kuhusu mboga za aina ya matunda.


Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walielewa kuwa nyanya ni mboga inayohifadhi chakula chake kwenye matunda na huweza kuliwa bila kupikwa au ikiwa imepikwa. Nyanya hutumika kama kiungo kwenye chakula, achali, kachumbari na vinywaji.

**Swali la 9:** Mboga za aina ya mizizi (        )

Swali hili lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kubaini mboga za aina ya mizizi.

Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa sababu jumla ya wanafunzi 323,238 (asilimia 34.01) walichagua G "karoti" ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 626,826 (asilimia 66.96) walichagua kati ya vipotoshi B "vitunguu saumu", C "viazi mviringo" na F "koliflawa". Aidha, jumla ya

wanafunzi 239 (asilimia 0.03) hawakujibu swali hili. Chati Na. 4 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 4:** Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 9 ulikuwa wa wastani.


Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za mboga. Wale waliochagua kipotoshi B "vitunguu saumu" na C "viazi mviringo" walidhani kuwa kwa vile mashina ya aina hizi za mboga huzalia mboga zake ardhini, basi zitakuwa ni aina ya mizizi. Wanafunzi waliochagua F "koliflawa" hawakuwa na uelewa kuhusu aina hii ya mboga. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mboga za aina ya mizizi.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu makundi ya mboga hivyo waliweza kubaini mboga za aina ya mizizi.

**Swali la 10:** Mboga za aina ya majani (        )

Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu mboga za aina ya majani.

Uchambuzi unaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa wanafunzi 591,628 (asilimia 62.26) walichagua jibu sahihi A "spinachi" wakati wanafunzi 358,453 (asilimia 37.72) walichagua kati ya vipotoshi B "vitunguu saumu", C "viazi mviringo", D "njegere", na E "nyanya". Jumla ya wanafunzi 219 (asilimia 0.02) hawakujibu swali hili. Chati Na. 5 inaonesha ufaulu wa wanafunzi katika swali hili.




**Chati Na. 5**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 10 ulikuwa mzuri.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mboga za aina ya majani. Hii ni kwa sababu mboga za spinachi zimezoeleka na hutumiwa na familia nyingi katika jamii, hivyo wanafunzi wengi wanazijua.

Wanafunzi waliochagua B “vitunguu saumu”, C “viazi mviringo”, D “njegere”, na E “nyanya” walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mboga hizi. Walifikiri kuwa mboga hizi zipo katika kundi la mboga za aina ya majani kwa kuwa baadhi ya watu hutumia majani yake kama mboga kutokana na tabia ya ulaji katika jamii husika. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mboga za aina ya majani.

**Swali la 11:** Mboga za aina za maua (        )

Swali hili lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu mboga za aina ya maua.

Jumla ya wanafunzi 352,484 (asilimia 37.1) walichagua jibu sahihi F “koliflawa” wakati wanafunzi 597,555 (asilimia 62.9) walichagua kati ya kipotoshi A “spinachi”, B “vitunguu saumu”, C “karoti”, D “njegere” na E “nyanya”. Wanafunzi 262 hawakujibu swali hili. Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 6**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 11.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 597,555 | 352,484 | 262 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 62.9 | 37.1 | 0 |

Wanafunzi waliochagua kati ya kipotoshi A “spinachi”, B “vitunguu saumu”, C “karoti” na E “nyanya” walikosa ujuzi wa kutosha wa kuainisha mboga za aina mbalimbali katika makundi makuu. Waliochagua D “njegere” walidhani kuwa njegere ni mboga za aina

ya maua kwa sababu mimea ya njegere hutoa maua yanayovutia ila walishindwa kutambua kuwa maua hayo sio mboga. Wanafunzi ambao hawakufanya swali hili walikosa maarifa kuhusu aina za mboga za aina ya maua.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walielewa kuwa sehemu ya koliflawa inayotumika kama mboga ni ua. Baadhi ya wanafunzi katika kundi hili pia walihusha neno maua kutoka kwenye swali katika Fungu A na neno flawa (linavyotamkwa katika lugha ya Kiingereza likimaanisha maua) kutoka kwenye neno koliflawa katika Fungu B.

**Swali la 12:** Mboga za aina ya mbegu (        )

Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutumia maarifa yao kuainisha mboga za aina ya mbegu.

Jumla ya wanafunzi 456,847 (asilimia 48.1) walichagua jibu sahihi D “Njegere”, wakati wanafunzi 493,235 (asilimia 51.9) walichagua B “vitunguu saumu”, C “viazi mviringo”, E “nyanya” na G “karoti”. Wanafunzi 215 hawakujibu swali hili. Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 7:** Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 12.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 493,235 | 456,847 | 215 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 51.9 | 48.1 | 0 |

Wanafunzi 493,235 waliochagua B “vitunguu saumu”, E “nyanya” na G “karoti” walikosa uelewa wa kutosha kuhusu mboga hizi. Walishindwa kuelewa kuwa mboga hizi zinatoa mbegu ndogondogo na haziliwi kama mboga. Waliochagua kipotoshi C “viazi mviringo” walidhani kuwa kwa vile viazi vyenyewe huwa vinapandwa na kuota kisha kuzaa viazi vingine, basi hivyo viazi vitakuwa ni mbegu. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walishindwa kuainisha makundi ya mboga.

Wanafunzi 456,847 waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mboga za aina ya mbegu ambazo ni jamii ya mikunde zinazojumuisha njegere, maharage, soya, dengu, mbaazi na kunde. Wanafunzi hawa hufundishwa kwa vitendo wanapokuwa shuleni hivyo walipata ujuzi wa kutosha kuhusu kundi hili la mboga.

**Swali la 13 – 15: Maswali ya kujaza nafasi zilizoachwa wazi**

**Swali la 13:** Faida ya kufuga kuku wa kienyeji ni kupata nyama na _________ ambavyo ni vyanzo vya protini.

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Kilimo*, *Ufugaji na Uvuvi*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu vyakula vya aina ya protini vinavyotokana na kuku. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida za ufugaji kuku katika lishe.

Jibu sahihi lilikuwa ni “mayai” na liliandikwa na wanafunzi 491,431 (asilimia 51.7). Jumla ya wanafunzi 458,522 (asilimia 48.3) waliandika jibu lisilo sahihi, wakati wanafunzi 215 hawakujibu swali


hili. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8.

**Jedwali Na. 8**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 13.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 458,522 | 491,431 | 347 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 48.3 | 51.7 | 0 |

Wanafunzi walioandika jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mazao ya chakula yanayotokana na ufugaji wa kuku wa kienyeji. Walielewa kuwa zaidi ya nyama, kuku pia hutoa mayai ambayo ni chanzo cha protini. Ufaulu mzuri wa wanafunzi hawa unaweza kuwa ulitokana pia na wanafunzi hao kushirikishwa au kuona shughuli za ufugaji wa kuku wa kienyeji katika familia zao. Kielelezo Na. 1 ni sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi.

**Kielelezo Na. 1**


13. Faida ya kufuga kuku wa kienyeji ni kupata nyama na mayai ambavyo ni vyanzo vya protini.

**Kielelezo Na. 1** ni sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi.

Wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu vyakula vya protini vinayotokana na kuku wa kienyeji. Kwa mfano, baadhi ya wanafunzi waliandika majibu kama maziwa, mbolea na fedha kwa kuwa walikosa uzoefu wa kufuga wanyama kutoka kwenye familia zao. Wanafunzi hawa walishindwa kuelewa kuwa jibu watakalolitoa ni lazima liwe ni zao la kuku ambalo pia ni chanzo cha protini. Wengine waliandika wali na chips vyakula ambavyo si vyanzo vya protini wala si mazao

yanayotokana na kuku. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu faida ya kufuga kuku wa kienyeji. Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 2.

**Kielelezo Na. 2**


> 13. Faida ya kufuga kuku wa kienyeji ni kupata nyama na MAZIWA. ambavyo ni vyanzo vya protini.

**Kielelezo Na. 2** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika maziwa ambayo hutokana na ng'ombe au mbuzi badala ya kuandika mayai ambayo hutokana na kuku.

**Swali la 14:** Vitambaa vya meza hurembwa kwa kutumia mishono ya ______________.

Swali hili lilitungwa kutoka katika mada ya *Ushoni wa Nguo*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi katika kubaini aina ya mishono inayotumika kuremba vitambaa. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu matumizi ya aina mbalimbali za mishono.

Jumla ya wanafunzi 151,656 (asilimia 15.96) waliandika "kutarizi" (au "kudarizi") ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 798,239 (asilimia 84) waliandika majibu yasiyo sahihi. Idadi ya wanafunzi ambao hawakujibu swali hili ni 409 (asilimia 0.04). Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa hafifu kama unavyoonakana kwenye Chati Na. 6.




**Chati Na. 6**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 14 ulikuwa hafifu.

Wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi hawakuweza kubainisha aina za mishono ya kuremba na matumizi yake. Baadhi ya wanafunzi hawa walitaja vifaa vinavyotumika katika ushonaji wa nguo kama vile mashine, sindano, uzi, na kitambaa. Baadhi ya wanafunzi katika kundi hili pia waliandika mifano ya mishono ya kutarizi/kuremba kama msalaba, mjazo na mnyororo badala ya kundi la mishono linaloitwa mishono ya kuremba. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na uelewa kuhusu aina za mishono ya kuremba inayotumika katika urembaji wa vitambaa. Kielelezo Na. 3 ni sampuli ya jibu la  mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 3**

14. Vitambaa vya meza hurembwa kwa kutumia mishono ya Uzi.

**Kielelezo Na. 3** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika uzi ambao ni moja ya vifaa vya kushonea badala ya kuandika kutarizi ambalo ni kundi la mishono itumikayo kuremba vitambaa vya meza.

Wanafunzi walioandika jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za mishono. Maarifa haya yaliwawezesha kutambua kuwa mishono ya kutarizi/kudarizi hutumika kuremba vitambaa vya meza. Baadhi ya wanafunzi hawa pia hulisikia neno hili au kushuhudia ushonaji huu kwa washonaji wa kudarizi ambao wamo katika mazingira wanamoishi. Kielelezo Na. 4 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 4**

14. Vitambaa vya meza hurembwa kwa kutumia mishono ya kutarizi.

**Kielelezo Na. 4** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi jibu la swali hili.

**Swali la 15:** Aina ya upishi inayotumika kutengeneza mikate huitwa ___________.

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Upishi*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu aina za mapishi. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina mbalimbali za mapishi ya vyakula.

Wanafunzi 223,393 (asilimia 23.51) waliandika “kuoka” ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 726,487 (asilimia 76.45) walishindwa kuandika jibu sahihi. Wanafunzi 421 (asilimia 0.04) hawakujibu

swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama unavyoonekana katika Jedwali Na. 9.

**Jedwali Na. 9**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 15.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 726,487 | 223,393 | 421 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 76.45 | 23.51 | 0.04 |

Wanafunzi walioandika jibu lisilo sahihi hawakuwa na dhana sahihi kuhusu njia mbalimbali za mapishi ya vyakula. Baadhi ya wanafunzi waliandika aina ya nafaka (ngano) inayosagwa na kutoa unga wa ngano ambao ni muhimu katika upishi wa mikate badala ya aina ya upishi. Wanafunzi wengine walitaja aina za mapishi kama kuchoma na kukaanga wakijua kuwa kwa vile upishi wa mikate hauhitaji maji basi utakua ni kati ya mapishi haya. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu aina za mapishi. Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi ni kama inavyoonekana katika Kielelezo Na. 5.

**Kielelezo Na. 5**

15. Aina ya upishi inayotumika kutengeneza mikate huitwa ngano.

**Kielelezo Na. 5** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika ngano ambayo ni nafaka inayotoa unga unaotumika kutengeneza mkate badala ya kuandika njia ya kupika mkate ambayo ni kuoka.

Wanafunzi walioandika jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu njia mbalimbali za mapishi. Wanafunzi hawa waliweza kutofautisha upishi wa mikate na mapishi ya aina nyingine za vyakula yasiyotumia maji kama kuchoma na kukaanga. Kielelezo

Na. 6 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 6**

15. Aina ya upishi inayotumika kutengeneza mikate huitwa Kuoka.

**Kielelezo Na. 6** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika kwa usahihi jibu la swali hili.

## 2.2 Sehemu B: Haiba na Michezo

**Swali la 16 - 22: Maswali ya kuchagua jibu sahihi**

**Swali la 16:** Watu hufanya mawasiliano ili

A kuwapatia watu wengine taarifa
B kusalimiana na watu kwa kuongea
C kujenga moyo wa kufanya kazi kwa pamoja
D kuvitumia vifaa vya mawasiliano.

Swali lililenga kupima uelewa wa mwanafunzi kuhusu sababu za kufanya mawasiliano. Swali lilitoka katika mada ya *Mawasiliano*, *Uhusiano na Ushirikiano*. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu faida za mawasiliano katika jamii.

Jumla ya wanafunzi 657,729 (asilimia 69.2) walichagua jibu sahihi A “kuwapatia watu wengine taarifa” wakati wanafunzi 292,477 (asilimia 30.8) walichagua kati ya vipotoshi B “kusalimiana na watu kwa kuongea”, C “kujenga moyo wa kufanya kazi kwa pamoja” na D “kuvitumia vifaa vya mawasiliano”. Hata hivyo, wanafunzi 91

hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa mzuri kama unaovyoonekana katika Jedwali Na. 10.

**Jedwali Na. 10**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 16.

| Alama | Waliokosa | Waliopata | Wasiojibu |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 292,477 | 657,729 | 91 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 30.8 | 69.2 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu lengo la mawasiliano. Hii inaweza kutokana na ukweli kuwa wanafunzi kama watu wengine hupata na hutoa taarifa kwa watu wengine kupitia njia mbalimbali za mawasiliano kama radio, maandishi, magazeti na kuongea kwa mdomo. Jambo hili liliwasaidia wanafunzi kupata jibu sahihi.

Kwa upande mwingine, wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi walikosa maarifa ya kutosha kuhusu mawasiliano. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi B “kusalimiana na watu kwa kuongea” walishindwa kubaini kuwa hii ni moja ya njia za mawasiliano (njia ya maongezi) na wala si sababu ya mawasiliano. Wanafunzi waliovutiwa na kipotoshi D “kuvitumia vifaa vya mawasiliano” walishindwa kubaini kuwa vifaa hivyo vinatumika ili kufanya mawasiliano na wala si sababu ya kufanya mawasiliano. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sababu za kufanya mawasiliano.

**Swali la 17:** Faida ya ubunifu ni

A uumbaji wa vifaa mbalimbali

B kukuza vipaji vya watu

C kujishughulisha katika kazi

D kuweza kununua vifaa vya ubunifu.

Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu faida ya ubunifu katika jamii. Swali hili lilitoka katika mada ya *Ubunifu*, *Ujasiliamali na Raslimali*. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya ubunifu na jinsi jamii inavyofaidika kutokana na ubunifu.

Wanafunzi 300,072 (asilimia 31.6) walichagua jibu sahihi B “kukuza vipaji vya watu” wakati wanafunzi 650,145 (asilimia 68.4) walichagua kati ya vipotoshi “A” uumbaji wa vifaa mbalimbali”, C “kujishughulisha katika kazi” na D “kuweza kununua vifaa vya ubunifu”. Aidha, wanafunzi 82 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 11.

**Jedwali Na. 11:** Idadi na silimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 17.

| Alama | Waliokosa | Waliopata | Wasiojibu |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 650,145 | 300,072 | 82 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 68.4 | 31.6 | 0 |

Wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuwa na dhana sahihi kuhusu maana ya neno ubunifu. Waliochagua kipotoshi ‘A” uumbaji wa vifaa mbalimbali” walivutiwa na neno “uumbaji” kwa kuelewa kuwa ubunifu unaendana na uumbaji na utengenezaji wa

vifaa vipya. Waliovutiwa na kipotoshi “C” “kujishughulisha katika kazi” na D “kuweza kununua vifaa vya ubunifu” walidhani kuwa ubunifu ni kazi kama zilivyo kazi nyingine hivyo utamwezesha mhusika kupata kipato kitakachomsaidia kununua vifaa vya kuunda vitu vipya. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya ubunifu.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya ubunifu. Walielewa kuwa ubunifu huhusisha uchunguzi, namna ya kujenga wazo au taswira kwa kufikiri kisha kuliweka kwenye maandishi au vitendo ili kuunda vitu vipya. Wanafunzi hawa walijua kuwa ubunifu unaonesha vipaji vya watu na unasaidia kukuza vipaji vya watu wengine katika jamii.

**Swali la 18:** Riadha ni mchezo unaojumuisha

A mbio fupi na mbio ndefu
B kutupa tufe na kisahani
C kuruka chini na kuruka juu
D mbio, miruko na mitupo.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uchezaji wa Michezo ya Riadha*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi kutumia maarifa waliyonayo kubaini aina za michezo ya riadha. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina mbalimbali za michezo na jinsi inavyochezwa.

Jumla ya wanafunzi 338,112 (asilimia 35.6) walichagua jibu sahihi D “mbio, miruko na mitupo” ambapo wanafunzi 612,120 (asilimia 64.4) walichagua kati ya vipotoshi A “mbio fupi na mbio ndefu”, B “kutupa tufe na kisahani”, na C “kuruka chini na kuruka juu”.

Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili ni 69. Jedwali Na. 12 linaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 12:** Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 18.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 612,120 | 338,112 | 69 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 64.4 | 35.6 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu lisilo sahihi hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya riadha. Wanafunzi hao hawakuelewa kuwa riadha si mchezo mmoja bali ni vikundi vitatu vya michezo ya kukimbia, kuruka na mitupo. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa uelewa kuhusu michezo ya riadha.

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walielewa kuwa riadha si mchezo mmoja bali unajumuisha michezo ambayo huweza kufanyika katika viwanja vya pamoja lakini kila mchezo kwa muda wake au katika eneo lake.

**Swali la 19:** Njia ya kukabili mienendo hatarishi ni pamoja na

A kupita chini ya nyaya za umeme

B kuvaa viatu

C kucheza barabarani

D kucheza katika majalala ya taka.

Swali lilitungwa kutoka katika mada ya *Matatizo na Matendo Hatarishi*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi kutumia maarifa yao kuzuia au kujikinga na madhara yatokanayo na mienendo hatarishi. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa

usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu vitu na mienendo ambayo ni hatari na njia za kuzuia madhara.

Jumla ya wanafunzi 364,552 (asilimia 38.4) walichagua jibu sahihi B "kuvaa viatu" wakati wanafunzi 585,661 (asilimia 61.6) walichagua kati ya vipotoshi A "kupita chini ya nyaya za umeme", C "kucheza barabarani" na D "kucheza katika majalala ya taka". Jumla ya wanafunzi 88 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama inaonekana katika Jedwali Na. 13.

**Jedwali Na. 13**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 19.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 585,661 | 364,552 | 88 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 61.6 | 38.4 | 0 |

Wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuelewa maelekezo ya swali. Wanafunzi hawa walidhani kuwa walitakiwa kuchagua mienendo ambayo ni hatarishi wakati swali lilitaka wachague njia ya kukabili mienendo hatarishi kama vile kupita chini ya nyaya za umeme, kucheza barabarani na kucheza jalalani. Moja ya njia za kukabili mienendo hii ni kuvaa viatu. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu madhara ya mienendo hatarishi na njia sahihi za kuyazuia.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya matatizo na mienendo hatarishi. Walielewa kuwa tabia ya kuvaa viatu ni njia mojawapo ya kuzuia miguu isijeruhiwe na vitu vyenye ncha kali. Wanafunzi hawa

walichagua jibu sahihi huenda kwa sababu walitumia uzoefu walioupata kutoka kwenye jamii wanamoishi wa sababu mara nyingi huvaa viatu wanapokuwa wakijishughulisha na kazi za nje ya nyumba.

**Swali la 20:** Tendo linalooonesha uamuzi wa busara ni

A kuomba ushauri kabla ya kuamua

B kuomba ushauri baada ya kuamua

C kuomba ushauri wakati wa kuamua

D kufuata uamuzi wa watu wengi.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Fikra Sahihi, Uamuzi wa Busara na Mpango Mzuri*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu wakati sahihi wa kuomba ushauri katika kufanya maamuzi. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uamuzi wa busara.

Jumla ya wanafunzi 474,755 (asilimia 50) walichagua jibu sahihi A “kuomba ushauri kabla ya kuamua” wakati wanafunzi 475,455 (asilimia 50) walichagua kati ya vipetoshi B “kuomba ushauri baada ya kuamua”, C “kuomba ushauri wakati wa kuamua” na D “kufuata uamuzi wa watu wengi”. Swali hili halikujibiwa na wanafunzi 88. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 14.

**Jedwali Na. 14**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 20.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 475,455 | 474,755 | 88 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 50 | 50 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya kufanya uamuzi. Walielewa kuwa uamuzi utaonekana mzuri au wa busara endapo ushauri utaombwa kabla ya kuamua.

Wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya uamuzi wa busara. Kwa mfano, waliochagua kipotoshi B "kuomba ushauri baada ya kuamua" na C "kuomba ushauri wakati wa kuamua" hawakujua muda sahihi wa kuomba ushauri. Waliovutiwa na kipotoshi D "kufuata uamuzi wa watu wengi" huenda ilichangiwa na usemi wa "wengi wape". Aidha, wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuwa na uelewa kuhusu uamuzi wa busara.

**Swali la 21:** Faida ya kulinda na kutunza mwili ni

A kuwa na mafuta mengi mwilini
B kuwa na utulivu wa akili
C kuwa na virutubisho vya ziada mwilini
D kuzuia kifo.

Swali lilitoka katika mada ya *Kulinda na Kutunza Afya*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu umuhimu wa kulinda na kutunza mwili. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi,

walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mambo yanayosaidia kuboresha afya ya akili.

Jumla ya wanafunzi 269,761 (asilimia 28.4) walichagua jibu sahihi B “kuwa na utulivu wa akili” wakati wanafunzi 680,456 (asilimia 71.6) walichagua kati ya vipotoshi A “kuwa na mafuta mengi mwilini”, C “kuwa na virutubisho vya ziada mwilini” na D “kuzuia kifo”. Wanafunzi 79 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama inanyoonekana kwenye Jedwali Na. 15.

**Jedwali Na. 15**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 21.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 680,456 | 269,761 | 79 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 71.6 | 28.4 | 0 |

Wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi walikuwa na uelewa mdogo kuhusu afya ya mwili. Waliochagua kipotoshi A “kuwa na mafuta mengi mwilini” na C “kuwa na virutubisho vya ziada mwilini” walishindwa kuelewa kuwa haya ni madhara ya kushindwa kulinda na kutunza mwili. Kuwa na mafuta na virutubisho vya ziada mwilini husababishwa na tabia ya ulaji usio wa afya au ukosefu wa mazoezi. Wale waliochagua kipotoshi D “kuzuia kifo” walishindwa kuelewa kuwa kulinda na kutunza mwili kunapunguza tu vifo na si kuzuia. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walishindwa kubainisha faida za kulinda na kutunza mwili.

Kwa upande mwingine, wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu afya ya mwili. Wanafunzi hawa

walielewa kuwa mwili unapolindwa na kutunzwa unakuwa na afya ambayo husababisha utulivu wa akili.

**Swali la 22:** Vipindi viwili vya mchezo wa mpira wa miguu vina jumla ya

A dakika 70

B dakika 45

C dakika 80

D dakika 90.

Swali lilitoka katika mada ya *Uchezaji wa Michezo ya Mpira*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu muda unaotumika kucheza mpira wa miguu. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sheria na kanuni za kucheza mpira wa miguu.

Jumla ya wanafunzi 513,480 (asilimia 54) walichagua jibu sahihi D "dakika 90" wakati wanafunzi 436,732 (asilimia 46) walichagua kati ya vipotoshi A "dakika 70", B "dakika 45" na C "dakika 80". Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili ni 86. Ufaulu wa jumla wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 16.

**Jedwali Na. 16**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 22.

| Alama | Waliokosa | Waliopata | Wasiojibu |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 436,732 | 513,480 | 86 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 46 | 54 | 0 |

Wanafunzi waliochagua jibu sahihi walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mchezo wa mpira wa miguu. Wanafunzi hawa walielewa kuwa mchezo wa mpira wa miguu una vipindi viwili na kila kipindi kinachezwa kwa dakika 45 ambazo hufanya jumla ya dakika 90. Wanafunzi hawa huenda wanapata habari za mchezo huu ambao unafahamika sana kutoka kwenye vyombo vya habari au hushiriki kuucheza wakati wa vipindi vya michezo shuleni.


Hata hivyo, wanafunzi walioshindwa kuchagua jibu sahihi hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mchezo wa mpira wa miguu. Kwa mfano, wanafunzi waliochagua kipotoshi A "dakika 70" na C "dakika 80" wanaonesha kutokuwa na ujuzi wa kanuni za mchezo wa mpira wa miguu. Inawezekana kuwa wanafunzi hawa hawashiriki kucheza mpira wa miguu kutokana na uhaba wa viwanja na vifaa vya michezo shuleni na majumbani. Wanafunzi waliochagua kipotoshi B "dakika 45" walishindwa kuelewa kuwa huo ni muda wa kipindi kimoja cha mchezo huo. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuelewa muda wa kucheza mpira wa miguu.

**Swali la 23 – 25: Maswali kujaza nafasi zilizoachwa wazi**

**Swali la 23:** Mchezo unaohusisha kujisawazisha, kujitoma, na kujifyatua unaitwa _________________.

Swali lilitoka katika mada ya *Jimnastiki*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu uchezaji wa michezo ya jimnastiki. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu aina za mazoezi yanayofanyika katika uchezaji wa michezo ya jimnastiki.

Wanafunzi 141,395 (asilimia 14.88) waliandika “jimnastiki” ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 808,618 (asilimia 85.09) walishindwa kuandika jibu sahihi. Hata hivyo, wanafunzi 286 hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa hafifu kama inavyoonekana katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 23 ni hafifu.

Wanafunzi wengi walishindwa kuandika jibu sahihi kwa kuwa walikosa uelewa kuhusu mchezo huu. Hii inaweza kutokana na kukosekana kwa mazoezi ya vitendo na kukosa walimu wa kutosha wenye uzoefu katika mchezo huu ambao sio maarufu hapa nchini. Wanafunzi walio wengi walitaja majina ya michezo mingine kama vile mpira wa pete, mpira wa miguu na rede. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa uelewa kuhusu mchezo wa jimnastiki. Kielelezo Na. 7 ni sampuli ya mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 7**

| |
|---|
| 23. Mchezo unaohusisha kujisawazisha, kujitoma na kujifyatua unaitwa Mpira wa Miguu. |

**Kielelezo Na. 7** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika jibu la mchezo maarufu wa mpira wa miguu badala ya jimnastiki.

Wanafunzi wachache (asilimia 14.88) waliweza kuandika jibu sahihi kuonesha kuwa walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu aina za mazoezi katika mchezo wa jimnastiki na jinsi yanavyofanywa. Wanafunzi hawa walielewa kuwa kujisawazisha, kujitoma na kujifyatua ni mifano ya mazoezi ya jimnastiki. Kielelezo Na. 8 ni sampuli ya mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 8**

| |
|---|
| 23. Mchezo unaohusisha kujisawazisha, kujitoma na kujifyatua unaitwa JIMNASTIKI. |

**Kielelezo Na. 8** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi jibu la swali hili.

**Swali la 24:** Mchezo wa *rede* huchezwa kwa kutumia __________________.

Swali lilitoka katika mada ya *Uchezaji wa Michezo Sahili*. Swali lililenga kupima uwezo wa wanafunzi wa kubaini kifaa muhimu cha kuchezea *rede.* Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uzoefu wa kucheza michezo ya rede.

Jumla ya wanafunzi 398,123 (asilimia 41.9) waliweza kuandika "mpira" ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 551,972 (asilimia 58.1) walishindwa kuandika jibu sahihi. Idadi ya wanafunzi ambao hawakujibu swali hili ni 190. Jedwali Na. 17 linaonesha kuwa ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa wa wastani.

**Jedwali Na. 17**: Idadi na asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama katika swali la 24.

| **Alama** | **Waliokosa** | **Waliopata** | **Wasiojibu** |
|---|---|---|---|
| **Idadi ya wanafunzi** | 551,972 | 398,123 | 190 |
| **Asilimia ya wanafunzi** | 58.1 | 41.9 | 0 |

Wanafunzi walioshindwa kuandika jibu sahihi hawakubaini kifaa muhimu kinachotumika kucheza *rede*. Wanafunzi wengi katika kundi hili walitaja vifaa kama vijiti, chupa, mawe na mchanga ambavyo hutumika kulingana na aina ya mchezo wa *rede* unaochezwa. Wengine waliandika aina za mipira kama mpira wa miguu na mpira wa pete ambayo kiuhalisia haiwezi kutumika katika kucheza mchezo huu. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili hawakuelewa jinsi mchezo wa *rede* unavyochezwa. Kielelezo Na. 9 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi.


**Kielelezo Na. 9**

24. Mchezo wa *rede* huchezwa kwa kutumia Vijiti.

**Kielelezo Na. 9** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika vijiti badala ya mpira.

Wanafunzi walioweza kuandika jibu sahihi huenda wanashiriki kucheza mchezo wa *rede*. Walitambua kuwa ili mchezo wowote wa rede uweze kuchezwa, mpira ni lazima utumike na vifaa vingine kama chupa na mchanga, vijiti na kokoto hutumika kulingana na aina ya mchezo wa rede unaochezwa. Kielelezo Na. 10 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 10**



24. Mchezo wa *rede* huchezwa kwa kutumia mpira.

**Kielelezo Na. 10** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kubaini kuwa mpira ndio jibu sahihi kwani unatumika katika aina zote za michezo ya *rede*.

**Swali la 25:** Hali ya kujali na kuheshimu watu hujulikana kama __________.

Swali hili lilitoka katika mada ya *Maadili na Utu*. Swali lililenga kupima uelewa wa wanafunzi kuhusu dhana ya utu. Ili wanafunzi waweze kujibu swali hili kwa usahihi, walitakiwa kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu tabia zinazoashiria utu wa mtu katika jamii.

Jumla ya wanafunzi 81,896 (asilimia 8.62) waliandika “utu” ambalo ni jibu sahihi wakati wanafunzi 867,789 (asilimia 91.32) walishindwa kuandika jibu sahihi. Hata hivyo, wanafunzi 601 (asilimia 0.06) hawakujibu swali hili. Ufaulu wa wanafunzi katika swali hili ulikuwa ni wa chini zaidi katika upimaji huu kama inavyoonekena katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8**: Asilimia ya wanafunzi waliokosa na waliopata alama inaonesha kuwa ufaulu katika swali la 25 ni hafifu.

Wanafunzi wengi (asilimia 91.32) walishindwa kuandika jibu sahihi kutokana na kukosa maarifa ya kutosha kuhusu dhana ya utu. Wanafunzi wengi katika kundi hili waliandika tabia kama utii, heshima, maadili na upendo. Walioandika heshima, utii na upendo walishindwa kuelewa kuwa haya ni matendo au tabia zinazoashiria utu wa mtu. Wale walioandika maadili walishindwa kutofautisha kati ya maadili na utu kwa vile yote yapo kwenye mada moja. Wanafunzi ambao hawakujibu swali hili walikosa maarifa kuhusu mada hii. Kielelezo Na. 11 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kuandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 11**

25. Hali ya kujali na kuheshimu watu hujulikana kama heshima.

**Kielelezo Na. 11** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika heshima badala ya utu.

Kwa upande mwingine, wanafunzi wachache (asilimia 8.62) walioandika jibu sahihi walikuwa na uelewa kuhusu dhana ya utu. Wanafunzi hawa waliyaelewa matendo au tabia zinazoashiria utu wa mtu katika jamii. Kielelezo Na. 12 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika jibu sahihi.

**Kielelezo Na. 12**

25. Hali ya kujali na kuheshimu watu hujulikana kama utu.

**Kielelezo Na. 12** ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeweza kuandika kwa usahihi jibu la swali hili.

## 3.0 TATHMINI YA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA MADA

Uchambuzi wa matokeo ya upimaji wa Masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne wa mwaka 2015 kwa kila mada unaonesha kuwa ufaulu wa jumla wa wanafunzi ulikuwa wa wastani.

Uchambuzi huu umeonesha kuwa mada ambazo wanafunzi walikuwa na ufaulu mzuri ni Udobi (asilimia 85.3), Mawasiliano, Uhusiano na Ushirikiano (asilimia 69.2) na Sanaa za Maonyesho (asilimia 64.1).

Wanafunzi walikuwa na ufaulu wa wastani katika mada za Uchezaji wa Michezo ya Mpira (asilimia 54), Fikra Makini, Uamuzi wa Busara na Mpango Mzuri (asilimia 50), Kilimo, Ufugaji na Uvuvi (asilimia 45.7), Ususi (asilimia 45), Uchezaji wa Michezo Sahili (asilimia 41.9), Upishi (asilimia 39.1), Matatizo na Matendo Hatarishi (asilimia 38.4), Uchezaji wa Michezo ya Riadha (asilimia 35.6), Ushoni wa Nguo (asilimia 33.2), Muziki (asilimia 32.9), Ubunifu, Ujasiliamali na Raslimali (asilimia 31.6), Kulinda na Kutunza Ufya (asilimia 28.4) na Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo (asilimia 23.9), .

Uchambuzi zaidi umeonesha kuwa mada ambazo wanafunzi walikuwa na ufaulu hafifu ni Jimnastiki (14.9%) na Maadili na Utu (8.6%). Ufaulu wa mada katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne wa mwaka 2015 masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo umeoneshwa katika **Kiambatisho A** na **B** katika taarifa hii**.**

## 4.0 HITIMISHO

Uchambuzi wa maswali yaliyofanywa na wanafunzi umeonesha kuwepo kwa changamoto zilizochangia ufaulu hafifu ikiwa ni pamoja

na wanafunzi kukosa maarifa au kuwa na uelewa mdogo katika baadhi ya mada za masomo haya. Uelewa mdogo katika baadhi ya mada ulionekana kusababishwa na ufundishaji wa nadharia zaidi kuliko vitendo. Wanafunzi kushindwa kuelewa maelekezo ya maswali pia kulichangia kuwepo kwa ufaulu hafifu katika maswali mbalimbali ya masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo katika Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne (SFNA) wa mwaka 2015.

Uchambuzi wa kila swali katika mada zilizopimwa umeonesha kuwa jumla ya maswali matatu (14, 23 na 25) yalikuwa na ufaulu hafifu, maswali kumi na nane (1, 2, 3, 4, 5, 8, 9, 11, 12, 13, 15, 17, 18, 19, 20, 21, 22 na 24) yalikuwa na ufaulu wa wastani na maswali manne (6, 7, 10, na 16) yalikuwa na ufaulu mzuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha ufaulu katika masomo ya Stadi za Kazi, Haiba na Michezo inapendekezwa mambo yafuatayo yazingatiwe:

(a) Walimu wahakikishe kuwa mada zote zilizoainishwa katika mihtasari ya masomo ya Stadi za Kazi na Haiba na Michezo zinafundishwa ipasavyo kwa kutumia mbinu sahihi za kuwashirikisha wanafunzi.

(b) Halmashauri za Wilaya zihakikishe kuwa viwanja na maeneo ya kuchezea yanatengwa ili kuwawezesha wanafunzi kushiriki katika michezo shuleni na nyumbani.

(c) Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi na Idara ya Uthibiti Ubora wa Elimu (TAMISEMI) wafuatilie na kuhakikisha kuwa mada zote zilizoainishwa katika mihutasari ya

masomo ya Stadi za Kazi na Haiba na Michezo zinafundishwa kikamilifu kwa kutumia mbinu stahili za kujifunzia.

(d) Walimu wawezeshwe kufundisha kwa vitendo zaidi kuliko nadharia ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kuelewa.

(e) Wanafunzi washauriwe kuhudhuria vipindi vyote na kufanya marudio ya mada zote zilizoainishwa katika mihtasari katika kipindi chote cha masomo na wakati wa kijiandaa kufanya upimaji wa kitaifa.

**Kiambatisho A**

**MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA KILA MADA NA SWALI KATIKA SOMO LA STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE 2015**

| Na. | Mada | Ufaulu kwa kila swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | % wa Ufaulu | | |
| 1 | Udobi | 7 | 85.3 | 85.3 | Mzuri |
| 2 | Mawasiliano, Uhusiano na Ushirikiano | 16 | 69.2 | 69.2 | Mzuri |
| 3 | Sanaa za Maonyesho | 6 | 64.1 | 64.1 | Mzuri |
| 4 | Uchezaji wa Michezo ya Mpira | 22 | 54 | 54 | Wastani |
| 5 | Fikra Makini, Uamuzi wa Busara na Mpango Mzuri | 20 | 50 | 50 | Wastani |
| 6 | Kilimo, Ufugaji na Uvuvi | 8 | 41.1 | 45.7 | Wastani |
| | | 9 | 34 | | |
| | | 10 | 62.3 | | |
| | | 11 | 37.1 | | |
| | | 12 | 48.1 | | |
| | | 13 | 51.7 | | |
| 7 | Ususi | 5 | 45 | 45 | Wastani |
| 8 | Uchezaji wa Michezo Sahili | 24 | 41.9 | 41.9 | Wastani |
| 9 | Upishi | 2 | 54.7 | 39.1 | Wastani |
| | | 15 | 23.5 | | |
| 10 | Matatizo na Matendo Hatarishi | 19 | 38.4 | 38.4 | Wastani |
| 11 | Uchezaji wa Michezo ya Riadha | 18 | 35.6 | 35.6 | Wastani |
| 12 | Ushoni wa nguo | 3 | 50.3 | 33.2 | Wastani |
| | | 14 | 16 | | |
| 13 | Muziki | 4 | 32.9 | 32.9 | Wastani |
| 14 | Ubunifu, Ujasiliamali na | 17 | 31.6 | 31.6 | Wastani |

| Na. | Mada | Ufaulu kwa kila swali | | Wastani wa ufaulu (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Namba ya swali | % wa Ufaulu | | |
| | Raslimali | | | | |
| 15 | Kulinda na Kutunza Afya | 21 | 28.4 | 28.4 | Wastani |
| 16 | Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo | 1 | 23.9 | 23.9 | Wastani |
| 17 | Jimnastiki | 23 | 14.9 | 14.9 | Hafifu |
| 18 | Maadili na Utu | 25 | 8.6 | 8.6 | Hafifu |

**Kiambatisho B**

## MUHTASARI WA UCHAMBUZI WA UFAULU WA WANAFUNZI KATIKA MADA MBALIMBALI KWA GRAFU KATIKA SOMO LA STADI ZA KAZI, HAIBA NA MICHEZO KATIKA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE 2015

